



Tarehe: 23/09/2020

## **YAH: TANGAZO LA ZABUNI**

### **ZABUNI YA UPANGISHAJI WA MAENEKO YA BIASHARA KATIKA SOKO LA KISASA LA CHUNO KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021**

1. Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara-Mikindani anapenda kuwaalika wananchi wote, Makampuni, Ushirika, Taasisi au vikundi vya watu vilivyo sajiliwa kisheria wenye nia ya kuwa wapangaji katika soko la kisasa la Chuno lenye maeneo ya kufanya biashara kama yafuatayo:-

Namba ya Zabuni	Eneo/aina ya biashara	Idadi	Ada ya Zabuni kwa kila moja
LGA/085/2020/2021//NC/09 LOT 1	Vizimba	306	Shilingi elfu kumi tu (10,000/=)
LGA/085/2020/2021/NC/09 LOT 2	Mabucha	6	Shilingi elfu hamsini tu (50,000/=)
LGA/085/2020/2021/NC/09 LOT 3	Migahawa	2	Shilingi elfu hamsini tu (50,000/=)
LGA/085/2020/2021/NC/09 LOT 4	Eneo la wazi la biashara	2	Shilingi elfu hamsini tu (50,000/=)
LGA/085/2020/2021/NC/09 LOT 5	Maeneo ya maduka	22	Shilingi elfu hamsini tu (50,000/=)
LGA/085/2020/2021/NC/09 LOT 6	Stoo	10	Shilingi elfu hamsini tu (50,000/=)

2.Maombi yote ya zabuni yazingatie masharti yafuatayo:-

- i. Maombi ya zabuni yaambatanishwe na nakala ya stakabadhi ya malipo kwa zabuni iliyoombwu iliyotolewa na Manispaa kuitia dirisha la malipo kwa mashine ya kielektroniki ya kukusanya mapato na malipo ya maombi hayo hayatarejeshwa.
- ii. Fomu ya maombi ya zabuni pamoja na nyaraka zingine za zabuni zinazopatikana ofisi ya Kitengo cha Manunuzi cha Manispaa zitakazojazwa na kusainiwa na mwenye uhalali wa kisheria iwapo muombaji ni Kampuni au Taasisi.
- iii. Mkataba wa upangishaji kwenye vizimba ni wa mwaka mmoja na kwenye maeneo yatakayohitaji ujenzi muda wa mkataba utategemea makubaliano ya mpangaji na mpangishaji.
- iv. Mwombaji asiwe anadaiwa na Halmashauri na asiombe kwa nia ya kumpangishia mtu mwingine.
- v. Waombaji wote wenye nia na uwezo wanaweza kupata ufanuzi kuhusiana na maeneo hayo toka kwa Mchumi wa Manispaa na Afisa Biashara wa Manispaa kila siku za Jumatatu,Jumatano na Ijumaa, kuanzia saa 8:00 mchana hadi saa 9:30 alasiri kuanzia tarehe ya tangazo hili.
- vi. Maombi yote yawekwe kwenye bahasha na kufungwa vizuri na iandikwe kwa Mkurugenzi wa Manispaa S.L.P 92 Mtwara na kuiwasilisha ofisi ya Kitengo cha Manunuzi ofisi kuu ya Halmashauri ya Manispaa.
- vii. Mwisho wa kupokea zabuni ni tarehe 06/10/2020 saa 5:00 asubuhi na ufunguzi utafanywa mara tu baada ya saa ya mwisho ya kupokea zabuni na wawakilishi wanaruhusiwa kuhudhuria ufunguzi huo.
- viii. Maombi ya zabuni yatakayochelawa kwa muda uliopangwa yatapokelewa na hayatafunguliwa.
- ix. Maelekezo yote yaliyotolewa katika tangazo hili na yaliyomo kwenye nyaraka za maombi ya zabuni ni sehemu ya masharti kwa waombaji zabuni.



COL. Emanuel Mwaigobeko  
**MKURUGENZI WA MANISPAA**  
**MTWARA-MIKINDANI**

**MKURUGENZI WA MANISPAA**  
**MTWARA - MIKINDANI**  
S. L. P 92  
**MTWARA**